**Mkutano Mkuu wa VI wa Wamisionari wa Upendo (Roma, 4-7 Oktoba 2022)**
***Tutembee pamoja ili kuwa ishara ya matumaini***

## Hati ya Mkutano

1 – *Safari yetu*

Katika muktadha wa kijamii, uliojaa wasiwasi, zaidi ya yote kwa sababu ya mivutano kati ya watu, na katika muktadha wa kikanisa, wenye sifa ya safari inayoendelea ya Sinodi (*Kwa ajili ya Kanisa la kisinodi: ushirika, ushiriki, utume*) na ya maandalizi kwa ajili ya Jubilei ijayo (*Wajaji katika matumaini*), iliwezekana kuadhimisha huko Roma, kwenye Makao Makuu ya Shirika, Mkutano Mkuu wetu wa VI (*Tutembee pamoja ili kuwa ishara ya matumaini*) kuanzia tarehe 4 hadi 7 Oktoba 2022.

Mkutano Mkuu ulipaswa kufanyika mwaka 2021, lakini uliahirishwa kwa sababu ya matatizo yaliyosababishwa na janga la Covid19; kwa idhini ya Idara ya Maisha ya Wakfu, tarehe 9 Juni 2022 (prot. 5428/2021), ulifanyika kwa mchanganyiko (yaani wengine walikuwepo Roma na wengine walihudhuria kupitia Zoom).

Hizi zilikuwa siku ambazo, licha ya mapungufu ya mawasiliano kupitia mtandao, tuliweza kuong'amua pamoja furaha ya wito na utume wetu katika Kanisa. Kwa hiyo tumefanya upya shukrani zetu na *ndiyo* yetu ya uhakika kwa mpango wa Mungu, kama Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili, tukifuata mfano wa Mama Antonia.

Kwa msingi wa kile kilichoangaziwa katika safari ya maandalizi, tuliangalia udhaifu wetu, lakini kuingizwa na wasiwasi wetu wa haki, sembuse "kufungwa" na mipaka yetu. Tumejitolea kwanza kumsikiliza Roho Mtakatifu, ili kutambua karama na wito unaoelekezwa kwa kila mmoja wetu na kwa Chama kizima, katika kipindi hiki cha Kanisa na cha ulimwengu. Kwa hiyo tumesoma udhaifu wetu wenyewe kwa kufahamu kwamba Roho Mtakatifu tayari anakuja kutusaidia katika udhaifu wetu (rej. *Rm 8:26-30*): anauchukua na kujimwilisha ndani yake, akiufanya kuwa "ishara" ya mpango wake na wito anaotuitia ili tushirikiane naye kwa ajili ya wokovu wa ulimwengu.

2 – *Viongozi wapya*

Tumeupyaisha Uongozi wa Chama na matokeo ya kura yametupatia viongozi hawa:

Rais : Ngeneka Scholastica
Makamu wa Rais na Mshauri wa kwanza: Mpore Lioba
Washauri wengine: Meo Maureen; Gambini Giuse; Corniello Annamaria.

3 – *Mapendekezo*

Kwa kupokea mapendekezo mliyoyatoa katika majibu ya dodoso, ttumetafakari juu ya vipengele muhimu kwa ajili ya maisha yetu na utume wetu.

Kwanza kabisa, ilionekana kuwa sawa kwetu kusisitiza juu ya hitaji la kila mmoja wetu na la Chama kizima kuimarisha safari yetu "pamoja na Yesu Mfufuka", ili mioyo yetu iweze kuwaka zaidi na zaidi kwa ajili yake (taz. *Lk. 24:13-35)*:

- Sala binafsi na ya kiliturujia,
- Kutafakari kwa makini neno la Mungu,
- Maisha ya kisakramenti
- Mafungo ikiwezekana miongoni mwetu na pamoja na watawa wengine, vipindi vya malezi miongoni mwetu, na kushiriki katika vile vya Kanisa mahalia.

Kwa namna ya pekee tumeona muhimu kusisitiza ushirikiano katika hatua za ziroho zinazopihwa na matawi mengine ua Familia ya kiverniani.

✓ Kwanza kabisa, lilijitokeza hitaji la kuongeza na kuimarisha *kule kutembea pamojas:*
- *kati yetu*, tukitumia vizuri fursa zote za mawasiliano na mkutano, hata mintarafu mtandao;
- *katika Kanisa mahalia*, tukishiriki kikamilifu, kadiri iwezekanavyo, safari ya kisinodi inayoendelea;
- *katika matawi mengine ya Familia ya kiverniana,* tukishirikiana kiroho, kidugu na kitume, hata katika upekee wa karama yak ila tawi.

✓ Wamisionari kadhaa waliangazia hamu na fursa ya maendeleo zaidi ya mienendo ya ushiriki na masista, katika ngazi zote.

✓ Ili kurahisisha *kutembea kwetu* pamoja, Mkutano Mkuu unatambua umuhimu wa kusasaisha mara kwa mara kitabu chenye data za Wanachama wote. Pia, inapendekeza maendeleo zaidi ya tovuti na uundaji wa gumzo la ndani kwa mawasiliano baina ya watu na taasisi

✓ Mkutano unapendekeza kwa Rais ajaye, kumuomba Mama Mkuu wa Shirika aweze kutupatia msaada wa kidugu wa sista mmoja katika kazi yake ya uhuishaji, kulingana na mbinu zilizokubaliwa.

Zaidi ya hayo, imesisitizwa umuhimu wa mapendekezo ya Katiba n°. 62.2 kuhusu uonekano wa Rais na Halmashauri yake.

- ✓ Kwa mustakabali wa Chama ni muhimu sana kujitolea zaidi kwa wote katika suala malezi.

Kwa ajili ya *malezi ya kwanza* ni muhimu kuzingatia kile kilichoandikwa katika Katiba n°68, kuhusu uchaguzi wa mwenye wajibu wa malezi. Inakumbukwa pia kuwa kila mpango wa malezi ni lazima uendane na hali ya mtu husika na muktadha wa kitamaduni.

Kwa ajili ya *malezi endelevu* esortiamo tutte tunahimiza kila mmja apitishe kwa uaminifu viashiria vya Katiba, ibara n° 84. Huku tukithamini mipango hata ya Kanisa mahalia, ni lazima kuanzisha tena mikutano yetu, katika ngazi mbali mbali, pia kwa kutumia njia za mawasiliano kupitia mitandao na katika ushirikiano na matawi mengine ya Familia ya kiverniana.

- ✓ Mwisho Mkutano Mkuu unasisitiza haja ya kutoficha zawadi tuliyopewa, bali kujua jinsi ya kuipendekeza pia kwa vizazi vipya. Hili si suala la kupiga debe, bali suala la kutoa ushuhuda wa maisha na kutangaza kwa ujasiri kuwa maisha ya wakfu yanasababisha uwezekano wa kutoa maana chanya na yenye furaha katika maisha; kwa ufupi, maana yake ni kuwa ishara ya matumaini, Mama Antonia alivyokuwa.

Kwa kumalizia, tunawakaribisha wote kuiga, licha ya shida na mapungufu, jibu la ujasiri la Petro: "*Mwalimu, tulifanya kazi kwa bidii usiku kucha bila kupata chochote, lakini kwa neno lako nitazishusha nyavu*" (Lk 5: 5).

Roma, 7 Oktoba 2022
Sikukuu ya Bikira Maria wa Rozari Takatifu

Kwa Wamisionari wa Upendo

N.K. Sr. Raffaella Giudici
Mama Mkuu

Mh. Vincenzo Fornace
Rais Mkuu Walei Wanaverniana
Corso Torino 107
10086 – Rivarolo

Mama Wakuu wa Provinsya na
jumuiya zote za kitawa

Wapendwa Wamisionari wa Upendo,

Tufurahi, kwani mara nyingine tena Bwana ametuonesha kuwa Chama chetu ni kazi yake. Yeye yuko pamoja nasi na anatembea nasi. Kwa hakika, kwa maombezi ya Mama Antonia, iliwezekana kufanya Mkutano wetu Mkuu wa VI uitwao ***"Tutembee pamoja ili tuwe ishara za Matumaini"*** ambao ulifanyika kuanzia tarehe 4 hadi 7 Oktoba 2022, huko Roma. Idadi ya Wamisionari waliokuwepo ilikuwa ndogo, lakini mtandao wa Zoom uliwezesha ushiriki kwa Wamisionari wengine Italia na ng'ambo: huko Yerusalemu, Argentina na Tanzania. ***Hati ya mwisho imeambatanishwa***.

Uchaguzi ulifanyika katika hali ya utulivu na kila wakati tulimwomba Roho Mtakatifu au Bikira Maria, tukiamini kuwa tunaweza kugundua, kwa kujitolea ipasavyo, Mapenzi ya Mungu juu yetu. Na, kama tu kwa mwale wa mwanga na matumaini ambao unatutia moyo wa kuendelea na safari kwa imani na shauku zaidi, mnamo tarehe 7 Oktoba, tulipata Uongozi mpya, ambao umeundwa kama ifuatavyo:

Rais: Scholastica Ngeneka
Makamu wa Rais na Mshauri wa kwanza: Lioba Mpore
Mshauri na Mhasibu: Giuse Gambini
Mshauri na Katibu: Annamaria Corniello
Mshauri: Maureen Meo

Safari ngumu ya sasa ya Chama lazima ituelekeze katika siku zijazo tukiwa na imani kuwa "Tumaini katika Mungu halikatishi tamaa kamwe". Tusiishie kwenye udhaifu unaosababishwa na umri mkubwa, umbali wa kijiografia, afya hatarishi; tabia hii, kadiri ya mtazamo wa Papa Francisko, *ni hali inayofanya maisha yetu ya wakfu kuwa tasa: kishawishi cha kuishi kijuu juu ambacho kinatufanya tuwe na hisia hasi, hofu, na kianchotufungandani ya nyumba zetu na mipango yetu. Na, badala ya kuamsha ubunifu wa kinabii, uliozaliwa kutokana na ndoto za Waanzilishi wetu, tunatafuta njia za mkato za kuepuka changamoto zinazobisha hodi kwenye milango yetu leo* (Rjea maneno ya Baba Mtakatifu katika *Siku ya Watatwa ya XXI*).

Kwa hivyo, tutazame ukakamavu wa Mama Antonia, "Hebu tuungane pamoja na Yesu kati ya watu wake" kama "mbegu na chachu", tukiwa na hamu ya kuishi "utakatifu katika hali yetu ya kilei". Kanisa "linalotoka" la Papa Francisko linatualika kuwa Mashahidi wanaovutia

wengine. Leo si wakati wa maneno, bali wakati wa ushuhuda. (*Ujumbe wa Papa Fransisko kwa washiriki wa Baraza wa Taasisi za Walei Wakfu zilizopo Italia, mwaka 2017*).

Tunamshukuru Luciana Tomasini, ambaye kwa moyo wa kishujaa ameongoza Chama kwa miaka 18; pia, tunamshukuru Padre Majorano, aliyetupa ujasiri mkubwa kwa uzoefu wake na usahihi wake; vile vile, tunasema asante kwa Mama Raffaella, ambaye siku zote yuko pamoja nasi akitusaidia na bidii na akili yake, pamoja na Mama Grazia ambaye anaendelea kutusindikiza kwa upendo wake wa dhati, bila kuwasahau Masista ambao walifanya kazi kama wakalimani, wakishiriki katika Mkutano Mkuu, kama sehemu ya familia kubwa.

Pengine Wamisionari wengine walitegemea kupata habari hizo kwa haraka zaidi. Tunaomba radhi kwa hilo, lakini ilibidi tuheshimu pia muda unaokimbia, nyajibu za kila siku, uzoefu wetu mdogo na pia magumu katika mawasiliano, kutokana na umbali.

Tunamaliza tukimwatakia kila mmoja safari ya kiroho ambayo iwe kama shamba la maua yanayochanua mapya kila mara. Tunatumaini kuwa mawasiliano ya mara kwa mara kati ya Wamisionari, Masista na Walei Wanaverniana wasaidie kuimarisha ndani yetu mwamko wa kuwa kama Familia kubwa ambayo inakua na kutembea ikielekea mustakhabali mzuri na wenye furaha. Tunategemea sala zenu ili tutekeleze vizuri utumishi wetu na tunawashukuru kwa kutuamini.

Salamu nyingi katika Kristo,

*Scholastica*
*pamoja na Lioba, Giuse, Maureen e Annamaria*